SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO BALOZI MOHAMED RAMIA ABDIWAWA (MBM) AKIWASILISHA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2019 NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2019/20

JUNI, 2019

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO BALOZI MOHAMED RAMIA ABDIWAWA (MBM) AKIWASILISHA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2019 NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2019/20

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Ni heshima ya kipekee ya kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/20. Naomba kuwasilisha Hotuba ya Mpango wa Maendeleo inayoambatana na Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2018 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019 na Kitabu cha Pili cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2019 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/20. Taarifa za vitabu hivyo zimezingatia Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar wa Awamu ya Tatu (MKUZA III) 2016-2020; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs) ya mwaka 2015-2030 pamoja na Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein aliyoitoa kwenye uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi.

2. **Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba wa vyote vilivyomo mbinguni na ardhini. Ni wajibu wetu tukiwa wanadamu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai, afya njema na uwezo wa kutekeleza majukumu yetu na kuweza kukutana tena leo kujadili masuala muhimu katika ujenzi wa Taifa letu kwa manufaa ya wananchi wote. Mwaka mmoja ni kipindi kikubwa kwa maisha ya binadamu, wako ambao wamepatwa na ugonjwa na wako ambao wametangulia mbele ya haki katika kipindi hiki. Namuomba Mwenyezi Mungu awasamehe wazee na ndugu zetu waliotangulia mbele ya haki na sisi tuliobakia atuzidishie afya njema, hekima na busara katika kujadili mijadala ya kikao hiki na vyengine. Atujaalie kheri, baraka na maelewano mazuri baina yetu, nguvu, utulivu, upendo na mshikamano miongoni mwetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Utulivu na amani katika nchi ni kitu muhimu sana na chenye thamani ya kipekee na inahitaji kulindwa kwa nguvu zetu zote. Kwa hili na kwa nafasi ya kipekee, nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi zake kubwa za kuhakikisha kuwa nchi yetu inabakia katika hali ya amani na utulivu kwa maslahi ya wananchi wote. Uongozi wake wa busara umesaidia kuimarika kwa uchumi na ustawi wa jamii kupitia huduma mbali mbali katika visiwa vya

Unguja na Pemba. Sisi sote ni mashahidi wa utekelezaji wa ufanisi mkubwa wa ahadi zake alizozitoa katika vikao na mikutano mbalimbali. Mfumo aliouanzisha Rais wetu wa ufuatiliaji kupitia bango kitita na mikutano ya mara kwa mara inamuwezesha kufahamu kwa karibu utekelezaji wa ahadi zake alizozitoa katika vikao na mikutano mbali mbali na kupelekea kupata mafanikio. Miongoni mwa shughuli alizozisimamia kwa nguvu zake zote ni pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya huduma za afya, elimu, maji, umeme, ujenzi wa barabara, na mawasiliano. Hatuna budi kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kuwa pamoja naye katika kuilinda na kuitunza miundombinu hiyo na rasilimali nyengine za nchi kwa manufaa ya wananchi wote na vizazi vijavyo.

4. **Mheshimiwa Spika**, Mafanikio haya yaliyopatikana yanatokana na ushirikiano mkubwa na wa karibu wa Msaidizi wake Mkuu, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa kumshauri vyema na kufanyakazi kwa karibu sana na Mheshimiwa Rais katika kuliendeleza Taifa na kutimiza jukumu lake la kusimamia shughuli za Serikali kwa umakini mkubwa. Kupitia fursa hii naomba pia kuwashukuru wajumbe wote wa Tume ya Mipango na Sekretariati yake kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kushauri, kutoa miongozo na maelekezo yao katika

uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Mipango Mikuu ya Maendeleo ya Kitaifa ikiwemo ya kiuchumi, uwekezaji na masuala ya kijamii. Maoni na maelekezo yao yanasaidia kwa kiasi kikubwa kuibua maeneo mapya ya kuyafanyia kazi kwa maslahi ya nchi yetu katika kuimarisha uchumi na kupunguza umasikini kwa wananchi wote. Tume ya Mipango chini ya Mwenyekiti wake Rais wa Zanzibar imefanya kazi kubwa ya kuendeleza uchumi wa Zanzibar.

5. **Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa nikushukuru wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid kwa kusimamia na kuendesha vyema vikao vya Baraza letu kwa ufanisi mkubwa. Hii inaonesha wazi ujasiri na umahiri ulionao katika kuendesha shughuli za Baraza. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima, busara na uweledi katika utendaji wa kazi zako za kila siku. Napongeza pia ushirikiano madhubuti, hekima na busara tunazozishuhudia kutoka kwa wasaidizi wako wakiwemo Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi na Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Sheha Hamad Mattar, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi. Kwa uzito huo huo, namshukuru sana Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed (Dimwa), Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi na Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara. Wote hawa ni nguzo muhimu sana katika mafanikio haya.

6. **Mheshimiwa Spika**, Naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuniteua mnamo mwezi Aprili mwaka 2019 na kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango. Naelewa kwamba jukumu hili la kuwatumikia wananchi wa Zanzibar nikiwa Waziri wa Fedha na Mipango linahitaji hekima na busara pamoja na kufuata Sheria, Sera na miongozo iliyopo kwa maslahi ya nchi. Niahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa ufanisi kwa kuzingatia misingi na maadili ya nchi yetu nikitarajia mashirikiano mazuri kutoka kwenu. Pamoja na hayo, sitaisahau kuishukuru sana familia yangu kwa kuwa na mimi muda wote, kunipa moyo, kuniunga mkono na kunisaidia kufanikisha majukumu yangu ya kazi. Namuomba Mola Mtukufu aniwezeshe kuyatekeleza yote hayo kwa uadilifu na ufanisi zaidi na yakidhi mahitaji ya wananchi wa Zanzibar.

7. **Mheshimiwa Spika,** shukurani za kipekee naomba nimshukuru mtangulizi wangu Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed kwa juhudi alizozifanya kwa kipindi chote alichokuwa katika wadhifa huo. Niahidi kuyaendeleza yale yote mazuri aliyoyaanzisha na kutekeleza yale aliyoyaacha katika hatua za awali. Naamini kuwa watendaji tuliopo tutashirikiana kuyakamilisha kwa wakati na ufanisi

mkubwa ili kukuza uchumi wetu na kuongeza tija kwa jamii.

8. **Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba nianze kuwasilisha Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2018 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2018 hadi Machi mwaka 2019 pamoja na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/20.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2018

### Mwenendo wa Uchumi

#### *Hali ya Uchumi Duniani*

9. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar kama zilivyo nchi nyengine duniani tunafuatilia kwa karibu mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia. Kuimarika kwa uchumi wa dunia ni kiashiria muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi Duniani, Uchumi wa Dunia umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2017 kama ifuatavyo: -

i. Nchi Zilizoendelea zimeripotiwa kuwa na ukuaji wa uchumi kufikia wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2017;

ii. Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi ukuaji ulifikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2017;
iii. Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara uchumi ulikua kwa kasi ya wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2017;
iv. Nchi za Afrika ya Mashariki, kasi ya ukuaji kufikia wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2018 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2017;

**Mfumko wa Bei wa Dunia**

**10. Mheshimiwa Spika,** Zanzibar inategemea bidhaa kutoka nje kwa zaidi ya asilimia 40 zikiwemo bidhaa za mafuta na gesi kwa mahitaji ya kila siku. Kwa mwaka 2018, kasi ya mfumko wa bei duniani imepanda kidogo na kufikia asilimia 3.8 kutoka asilimia 3.2 mwaka 2017. Kupanda huko kumetokana na kupanda kwa bei za bidhaa na huduma kwa baadhi ya nchi duniani kama ifuatavyo: -

i. Mfumko wa bei wa nchi Zilizoendelea umepanda hadi kufikia asilimia 1.7 mwaka 2018 kutoka asilimia 1.2 mwaka 2017;
ii. Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi kasi ya mfumko wa bei imepanda hadi kufikia wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2018 kutoka wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2017;

iii. Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kasi ya mfumko wa bei imepanda na kufika asilimia 12.8 mwaka 2018 kutoka asilimia 11.0 mwaka 2017;
iv. Nchi za Afrika ya Mashariki kasi ya mfumko wa bei imepungua kufikia asilimia 5.2 mwaka 2018 kutoka asilimia 6.1 mwaka 2017.

**Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar**

**11. Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kueleza kwa ufupi mapitio ya viashiria vya uchumi kwa kipindi cha mwaka 2018. Viashiria vya mwenendo wa uchumi kwa ujumla wake vinaonesha kuwa uchumi wa Zanzibar ni imara. Katika mwaka 2018, Pato Halisi la Taifa lilikuwa TZS 2,874 bilioni ikilinganishwa na TZS 2,684 bilioni mwaka 2017, sawa na ukuaji wa asilimia 7.1, ambapo Pato la Taifa kwa bei za soko limefikia thamani ya TZS 3,663 bilioni mwaka 2018 kutoka thamani ya TZS 3,228 bilioni mwaka 2017. Ukuaji huu umeiwezesha Zanzibar kuendelea kuwa na kiwango cha juu cha ukuaji kwa nchi za Afrika ya Mashariki kwa mwaka 2017 na 2018. Ukuaji wa Uchumi kwa mwaka 2018 umetokana na mambo mbali mbali yakiwemo:

i. Kuongezeka kwa Idadi ya Watalii waliofika nchini kwa asilimia 20.1 kufikia watalii 520,809 mwaka 2018 kutoka watalii 433,474 mwaka 2017;

ii. Kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la Mwani na kufikia tani 18,215 zenye thamani ya TZS 9.1 bilioni mwaka 2018 ikilinganishwa na tani 12,017 zenye thamani ya TZS 3.9 bilioni mwaka 2017 sawa na ongezeko la thamani la asilimia 133;

iii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na kufikia jumla ya tani 323,170 sawa na thamani ya TZS 263.7 bilioni mwaka 2018 ikilinganishwa na tani 306,190 sawa na thamani ya TZS 236.2 bilioni mwaka 2017 sawa na ongezeko la thamani ya asilimia 11.6. Mazao yaliyoongezeka ni pamoja na Mpunga, Muhogo na Viazi vitamu;

iv. Kuongezeka kwa shughuli za sekta ndogo ya usafirishaji na uhifadhi mwaka 2018, ikiwemo kuongezeka kwa idadi ya abiria waliopitia bandarini kufikia abiria 2.7 milioni mwaka 2018 ikilinganishwa na abiria 2.6 milioni mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Aidha, idadi ya abiria waliopitia viwanja vya ndege nayo imeongezeka na kufikia abiria 1.4 milioni mwaka 2018 kutoka abiria 1.2 milioni mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Kasi ya ongezeko la ndege imekuwa nzuri na hasa kutokana na ndege nyingi zinazotumia kiwanja chetu cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume;

v. Kuongezeka kwa muda wa kukaa kwa mgeni (duration of stay). Jumla ya watalii 5,920 walikaa kwa siku 31 mwaka 2018 ikilinganishwa na watalii 5,046 waliokaa kwa siku kama hizo kwa mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 17.3;

vi. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini. Katika kipindi chote hiki tumeshuhudia kuwepo kwa amani na utulivu nchini mambo ambayo yametuwezesha kupata ufanisi katika kutekeleza mipango yetu ya maendeleo na kuimarisha huduma mbali mbali za kijamii.

**Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa**

**12. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Huduma iliendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa ikilinganishwa na sekta nyengine. Sekta hii hujumuisha shughuli za malazi na chakula, ukodishaji majengo, utawala wa umma, hoteli na mikahawa, biashara na ukarabati, usafiri na mawasiliano, afya, elimu, taasisi za kifedha, majengo na biashara na huduma nyengine. Katika mwaka 2018, Sekta ya Huduma ilichangia asilimia 51.3. Sekta hii inajumuisha utalii kwa ujumla ambapo sekta ndogo zilizoimarika ni pamoja na: Malazi na Chakula asilimia 19.5, Fedha na huduma za Bima asilimia 3.8, Ukodishaji majengo asilimia 8.2, na utawala wa umma asilimia 5.8. Aidha, Sekta ya Kilimo ni sekta ya pili

kwa kuchangia uchumi wa Zanzibar baada ya sekta ya Huduma. Sekta ya kilimo hujumuisha mazao, ufugaji, misitu na uvuvi. Mchango wa sekta ya kilimo kwa mwaka 2018 ulifikia wastani wa asilimia 21.3. Sekta ndogo ya mazao ilichangia asilimia 8.6, mifugo asilimia 6.1, misitu asilimia 1.3 na uvuvi asilimia 5.2.

13. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya viwanda bado ina mchango mdogo wa wastani wa asilimia 17.8 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na sekta nyengine. Sekta hii hujumuisha sekta ndogo ya ujenzi, uchimbaji mawe na mchanga, uzalishaji viwandani, umeme na gesi na nyenginezo. Sekta ndogo ya ujenzi ilichangia asilimia 9.5, uchimbaji mawe na mchanga asilimia 1.2 na uzalishaji viwandani asilimia 5.7.

## Idadi ya Watu na Pato la Mwananchi

14. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2018, Zanzibar ilikadiriwa kuwa na idadi ya watu 1,579,849. Kutokana na kuimarika kwa Pato la Taifa mwaka 2018, kipato cha mtu mmoja mmoja nacho kimeongezeka kutoka TZS 2,104,000 sawa na dola za Kimarekani 944 na kufikia TZS 2,323,000 sawa na dola za kimarekani 1,026. Bado kunahitajika msukumo zaidi wa kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa, hata hivyo kiwango hiki kinakaribia kufikia kiwango cha uchumi wa kipato cha kati cha dola za Kimarekani 1,040 kama lilivyo lengo la Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020.

## Mfumko wa bei Zanzibar

15. **Mheshimiwa Spika,** Mfumko wa bei bado umeendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani na kwa nchi jirani, kutoyumba kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia na utekelezaji wa Sera ya Serikali ya kupunguza matumizi. Wastani wa mfumko wa bei kwa mwaka 2018 ulikuwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2017. Mfumko wa bei wa bidhaa za chakula ulipungua kutoka asilimia 5.5 mwaka 2017 hadi asilimia 1.4 mwaka 2018 na mfumko kwa bidhaa zisizo za chakula umeshuka na kufikia asilimia 5.7 mwaka 2018 kutoka asilimia 5.8 mwaka 2017. Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiwango kikubwa na kushuka kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia na soko la ndani pamoja na kushuka kwa bidhaa za chakula kutokana na hali nzuri ya hewa. Matarajio ni kubaki na mfumko wa bei katika kiwango cha tarakimu moja kwa kuongeza uzalishaji wa ndani hususan wa chakula na kuimarisha Sera za kifedha.

16. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sababu na hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika kudhibiti mfumko wa bei ni pamoja na:

    i) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao makuu ya chakula. Jumla ya tani 323,170.2 zilivunwa kwa

mwaka 2018 ikilinganishwa na tani 302,190.4 mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 5.5;

ii) Kuendelea kuwawezesha wakulima kwa kutoa pembejeo na mafunzo juu ya kuongeza uzalishaji kwa kutumia teknolojia ya gharama nafuu;

iii) Kuendeleza tafiti katika sekta ya kilimo ili kupunguza na hatimae kutokomeza maradhi yanayokabili mazao ya matunda na mboga;

iv) Kuendelea kutoa nafuu maalum ya ushuru kwa baadhi ya bidhaa muhimu za chakula, dawa na pembejeo za kilimo;

v) Benki Kuu kuendelea kusimamia Sera za kifedha kwa lengo la kuongeza kiwango cha fedha katika Uchumi kwa kutoa mikopo kwa benki za biashara;

vi) Benki Kuu kuendelea kudhibiti sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine zenye nguvu.

**Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

17. **Mheshimiwa Spika,** Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kuwa tulivu kipindi chote cha mwaka 2018 ikilinganishwa na thamani ya sarafu za nchi nyengine duniani. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ilipungua kwa wastani wa asilimia 1.6 ikilinganishwa na asilimia 2.4

mwaka 2017. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 2,264 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,229 mwaka 2017. Kushuka kidogo kwa thamani ya shilingi kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi na kuimarika kwa Dola.

## Sekta ya Nje

### Biashara na Nchi za Nje

18. **Mheshimiwa Spika,** Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yalipungua kwa asilimia 60 katika mwaka 2018 na kufikia thamani ya TZS 58.2 bilioni mwaka 2018, kutoka TZS 145.7 bilioni mwaka 2017. Hali hii imetokana na kupungua kwa usafirishaji wa zao la karafuu kutoka tani 7,077 zenye thamani ya TZS 121.8 bilioni mwaka 2017 na kufikia tani 860 zenye thamani ya TZS 15.5 bilioni mwaka 2018. Tuelewe karafuu ni zao la msimu, hivyo kupanda na kushuka kwa uzalishaji kwa zao hili ni hali ya kawaida. Hata hivyo, zao la Mwani limeonesha matokeo tofauti ambapo usafirishaji wa zao hilo umeongezeka na kufikia tani 18,215 zenye thamani ya TZS 9.1 bilioni mwaka 2018 kutoka tani 12,017 zenye thamani ya 3.9 bilioni mwaka 2017; sawa na ongezeko la thamani la asilimia 133. Kwa upande mwengine thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi imeongezeka kwa asilimia 58.9 kutoka bidhaa zenye thamani TZS 211.4

bilioni mwaka 2017 kufikia TZS 335.8 bilioni mwaka 2018. Uagiziaji huo wa bidhaa unahusisha bidhaa kama vile vyombo vya moto na vipuri vyake, mashine, vifaa vya ujenzi na chakula.

**Mwenendo wa Utalii**

19. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta zilizo na mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Katika mwaka 2018 idadi ya watalii waliotembelea nchini iliongezeka kwa asilimia 20.1 kufikia watalii 520,809 kutoka watalii 433,474 mwaka 2017. Serikali iliendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, kuimarika kwa ulinzi katika maeneo ya kitalii na kufanya kazi kwa kushirikiana baina ya Sekta za Umma na binafsi. Aidha, jumla ya matamasha 7 yalifanyika nchini nayo ni: Tamasha la Zanzibar Tourism Show, Pemba Tourism Port Bonanza, Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari, Tamasha la Urithi wa Mtanzania, Tamasha la Maonesho ya Chakula na Mavazi, Tamasha la Sauti za Busara na Tamasha la Nchi za Jahazi (ZIFF).

**Miradi ya Mashirikiano baina ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)**

20. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya miradi 13 ya awamu ya kwanza inaendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu na

wataalamu elekezi wa Kampuni ya 'Intercontinental Consultants and Technocrats Ltd'. Miradi hiyo ni:

i. Ujenzi wa Kituo cha daladala Kijangwani;

ii. Ujenzi wa soko la Chuini;

iii. Ujenzi wa soko la Mwanakwerekwe;

iv. Ujenzi wa soko la Mombasa;

v. Ujenzi wa soko la Mkokotoni;

vi. Ujenzi wa soko la Jumbi;

vii. Ujenzi wa soko la Machomane;

viii. Ujenzi wa Kituo cha Maonesho ya Biashara na mikutano Fumba;

ix. Ujenzi wa Mabweni ya wanafunzi SUZA, Tunguu;

x. Ujenzi wa Maegesho ya gari Michenzani;

xi. Ujenzi wa Kituo cha daladala Chanjaani Chake Chake;

xii. Mradi wa nishati mbadala ya jua kwa majengo mapya ya Serikali;

xiii. Mradi wa kuchakata/kusarifu taka ngumu.

21. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, maombi ya wazabuni 16 yamepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya PPP kwa awamu ya pili. Mshindi katika zabuni hiyo anatarajiwa kufanya upembuzi yakinifu juu ya fursa ya kuwepo kwa miradi ya PPP katika sekta za utalii, viwanda na nishati.

**Maendeleo ya Sekta ya Fedha**

22. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Fedha ni moja ya sekta za kiuchumi ambayo imekuwa ikipata mafanikio makubwa katika kipindi cha hivi karibuni. Amana za benki ziliongezeka kwa asilimia 10 kwa kipindi cha mwaka mmoja kutoka TZS 797.5 bilioni mwishoni mwa mwezi wa Machi mwaka 2018 na kufikia TZS 873.5 bilioni kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2019. Hali hii inaashiria kuongezeka kwa watumiaji wa huduma za benki kutokana na uhamasishaji unaoendelea kufanywa na mabenki unaotokana na ushindani uliopo pamoja na kuanzishwa kwa benki zinazotoa huduma kwa mujibu wa maadili ya kiislamu ikiambatana na kuanzishwa kwa huduma za kibenki kupitia simu za mikononi.

23. **Mheshimiwa Spika,** Kufikia mwaka 2019 Zanzibar ina benki 12 ambazo zinatoa huduma nazo ni:- Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ); National Microfinance Bank (NMB); Diamond Trust Bank (DTB); Exim Bank; National Bank of Commerce (NBC); Equity Bank; National Industrial and Commercial Bank (NIC);

Amana Bank; Kenya Commercial Bank (KCB); Bank of Africa; Postal Bank; Barclays Bank. Kati ya Benki hizo, benki mbili ni mpya nazo ni Amana Bank na NIC.

24. **Mheshimiwa Spika,** sekta nyengine ni Sekta ya Bima ambayo inaonesha mafanikio siku hadi siku. Kwa sasa Zanzibar ina Kampuni sita zinazotoa huduma za Bima nazo ni:- Zanzibar Insurance Corporation; National Insurance Corporation; Jubilee Insurance Corporation; Sanlam Life Insurance Company, UAP Insurance Company na Mayfair Insurance Company. Halkadhalika, Shirika la Bima la Zanzibar linaendelea kutoa huduma zake kwa wananchi katika Ofisi zake mbili zilizopo Zanzibar na Ofisi sita zilizopo Tanzania Bara na kupitia kwa mawakala na madalali. Ofisi hizo ni: Mpirani Zanzibar; Kanda ya Pwani Dar es Salaam; Kanda ya Ziwa Mwanza; Kanda ya Kati Dodoma; Kanda ya Nyanda za juu Kusini Mbeya, Kanda ya Kaskazini Arusha; Kanda ya Kusini Mtwara; Kituo cha Mauzo Pemba na Kituo cha Mauzo Kijitonyama Dar es salaam.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA JULAI 2018 HADI MACHI 2019

25. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19 ni muendelezo wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza

Umasikini Zanzibar awamu ya tatu (MKUZA III). Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2018/19 ulilenga kutekeleza jumla ya programu 27 na miradi 55 yenye jumla ya TZS 613 bilioni ikiwa ni ongezeko la TZS 116.4 bilioni sawa na asilimia 23.4 ikilinganishwa na bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2017/18 ya TZS 496.6 bilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 148.8 bilioni sawa na asilimia 24.3 ya bajeti ya maendeleo kutoka fedha za ndani. Jumla ya TZS 464.2 bilioni sawa na asilimia 75.7 zilipangwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 75.6 bilioni ni ruzuku na TZS 388.6 bilioni ni mikopo.

Hadi kufikia Machi 2019, jumla ya TZS 254 bilioni zilitumika ikiwa ni sawa na asilimia 41 ya lengo la TZS 613 bilioni zilizopangwa kwa mwaka huu wa fedha katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS 72 bilioni sawa na asilimia 49 kutoka Serikalini na TZS 181 bilioni sawa na asilimia 39 zimetoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hata hivyo, jumla ya TZS 71.3 bilioni zimepatikana nje ya Mpango wa Maendeleo ikiwa TZS 2.9 bilioni zimetolewa kwa shughuli za kawaida na TZS 68.4 bilioni zimetolewa kwa ajili ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa uwanja wa Mao Tse Tung na mradi wa E-Government awamu ya pili.

## UTEKELEZAJI WA MAENEO YA VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA JULAI 2018 HADI MACHI 2019

26. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha utekelezaji wa MKUZA III unafanyika kwa ufanisi, miradi mbalimbali imetekelezwa kwa mujibu wa Mpango Kazi uliyopo. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, miradi mbalimbali imetekelezwa kupitia maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:-

    a. **Kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini**, **barabara na nishati**

27. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha miundombinu, ujenzi wa jengo jipya la abiria la uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzibar (*Terminal III*) umeendelea kwa matengenezo ya ndani ya jengo na eneo la nje la kuegeshea ndege. Mkanda wa mizigo (*conveyor belt*) umewekwa na mfumo wa baridi umefanyiwa matengenezo katika jengo la abiria linalotumika kwa sasa (*Terminal II*). Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani umeanza kwa uwekaji wa miundombinu muhimu na ya msingi ikiwemo barabara, maji na umeme pamoja na ulipaji fidia kwa wanakijiji na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya wananchi wa kijiji hicho cha Dundua. Mchakato wa kupata mkopo wa fedha kwa kufanya upembuzi yakinifu kwa ujenzi wa bandari ya Mangapwani na ujenzi wa matangi ya kuhifadhia mafuta umeanza.

**28. Mheshimiwa Spika**, Usafiri wa barabara umeimarishwa kwa kuendeleza ujenzi wa barabara za Bububu-Mahonda-Mkokotoni (km 31) ambapo ujenzi umefikia asilimia 44. Ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja yenye urefu wa kilomita 35 unaendelea ambapo jumla ya kilomita kumi na tatu na nusu (13.5 km) kutoka Ole mpaka Mwanamwari Pujini zishawekwa lami. Vile vile, kilomita moja kutoka Mwanamwari Pujini mpaka Skuli ya Pujini zishawekwa rojo, kilomita 2.8 kutoka Skuli ya Pujini mpaka Tangi la maji zishawekwa kifusi tabaka la tatu, kilomita 2.7 kutoka Tangi la maji mpaka Chambani zishawekwa kifusi tabaka la kwanza na usafishaji kwa eneo la kilomita kumi kutoka Chambani mpaka Kendwa unaendelea. Aidha ujenzi wa madaraja saba na makalavati 7 umekamilika. Barabara za Pale - Kiongele na Matemwe - Muyuni zimeanza kusafishwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi. Ujenzi wa barabara ya Chake Chake – Wete (km 22.1) umeanza kwa kufanya tathmini ya maeneo yatakayoathiriwa na ujenzi. Upembuzi yakinifu kwa barabara za Chake Chake-Mkoani (km 43.5), Tunguu-Makunduchi (km 48) na Fumba-Uwanja wa Ndege (km 12) umekamilika.

**29. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za umeme, upelekaji umeme katika kisiwa cha Uvinje umekamilika na jumla ya kaya 77 kati ya kaya 95 sawa na asilimia 81 ya kaya zote zilizomo katika kisiwa hicho tayari zimeunganishwa na huduma hiyo muhimu.

**b. Kuendeleza utalii kwa kuimarisha maeneo ya kihistoria**

30. **Mheshimiwa Spika,** Katika kukuza na kuimarisha utalii**,** maeneo ya Bikhole, Bungi na MwinyiMkuu- Dunga yamefanyiwa matengenezo makubwa ili kurudisha haiba na muonekano mzuri kama ulivyokuwa hapo awali. Matengenezo hayo kwa upande wa Bikhole yamehusisha ujenzi wa kuta, kurejesha madirisha ya asili, na kurejesha mfumo wa maji kama uliokuwepo awali. Aidha, Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii imeandaa mpango wa kuliimarisha zaidi eneo la Bikhole kwa kuweka vivutio vyengine vya kitalii. Katika eneo la Mwinyimkuu Dunga kuta zilizokuwepo awali zimerejeshwa na kurekebisha kuta zilizobomoka na kujenga upya kuta ambazo zilianguka kabisa. Eneo la Mkamandume limeanza kuimarishwa kwa kukifanyia matengenezo kisima cha wivu sambamba na kuanza ujenzi wa njia inayotoka baharini hadi kwenye jengo pamoja na ujenzi wa kuta tatu zilizokuwepo hapo awali. Kwa upande wa Fukuchani shughuli za ujenzi zimeanza pia. Matengenezo ya Beit El Ajab nayo yanaendelea pamoja na nyumba nyengine muhimu za Mji Mkongwe.

**c. Kuimarisha viwanda vidogo vidogo kwa kuongeza thamani za bidhaa**

31. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuongeza thamani za bidhaa, mafunzo ya kusarifu mwani kwa wakulima 45 yametolewa na wataalamu kutoka nchini Indonesia. Aidha, matengenezo ya majengo yaliyopo Maruhubi yamekamilika na sasa yanatumiwa na Ofisi ya Wakala wa kuendeleza Viwanda (SMIDA). Matayarisho ya ujenzi wa Ofisi na Vituo vya kanda na Mikoa yanaendelea. Halikadhalika, maeneo tengefu matatu yamepatikana ambayo ni Nungwi kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Dunga kwa Mkoa wa Kusini Unguja na Chamanangwe kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kazi ya kuyapima, kulipa fidia na kutayarisha ramani inaendelea. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa maabara na Ofisi za Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imekamilika na Awamu ya pili ya ujenzi inaendelea na utaratibu wa zabuni za kumpata mkandarasi.

**d. Kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji, uvuvi na mifugo**

32. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha uvuvi, ujenzi wa Soko la Samaki Malindi unaendelea kwa kuunganisha umeme kwa ajili ya matumizi ya soko hilo na kufunga mtambo wa barafu kwa ajili ya kuhifadhia samaki. Vile vile, Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) imekamilisha Utafiti wa Masoko ya Ndani na Nje ya Zanzibar kwa lengo la kukuza uvuvi wa kibiashara na kuendeleza nchi yetu katika uchumi wa buluu. Hatua

za ununuzi wa boti mbili za uvuvi nchini Srilanka zimekamilika na boti moja itawasili nchini baada ya wataalamu kuridhika na vigezo vya ujenzi wa boti hiyo. Aidha, Matengenezo ya miundombinu ya umwagiliaji maji yamefanyika katika mabonde ya Cheju (mita 400), Bumbwisudi (mita 60) na Mwera (mita 50). Ufungaji wa pampu mpya za maji katika bonde la Cheju pamoja na matengenezo ya mifumo ya umeme katika vibanda vitatu vya pampu za maji kwa maeneo ya Cheju, Mkanyageni na Kirindunda umekamilika kwa asilimia 100. Ujenzi wa karantini ya mifugo Nziwengi-Gando Pemba unaendelea na umefikia asilimia 60 hadi kukamilika.

**e. Kuimarisha ubora wa huduma za kijamii**

33. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha ubora wa elimu, jumla ya walimu 652 wanaendelea na mafunzo ambapo shabaha ilikuwa ni kusomesha walimu 600. Skuli mpya mbili zimezinduliwa zikiwemo ya Sekondari ya Bwefum na skuli ya Msingi Pangawe. Aidha, jumla ya madarasa 100 sawa na asilimia 100 yaliyoanzishwa na wananchi yamekamilishwa kwa Unguja na Pemba. Kati ya madarasa hayo, madarasa 60 ni ya skuli za msingi na 40 ni skuli za sekondari. Ujenzi wa skuli tisa za ghorofa za sekondari (Mwembeshauri, Kinuni, Fuoni, Bububu na Chumbuni kwa Unguja; Micheweni, Wara, Mwambe na Kizimbani kwa Pemba) umekamilika hatua inayoendelea ni uwekaji wa vifaa vya maabara ili yakabidhiwe rasmi Serikalini.

Ujenzi wa maabara kwa skuli 23 unaendelea sambamba na ujenzi wa Vituo vya Amali vya Makunduchi kwa Unguja na Daya Mtambwe kwa Pemba.

34. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa afya, Hospitali ya Kivunge imepandishwa daraja na kufikia hadhi ya Wilaya kwa kuendeleza majengo na uwekaji wa vifaa vya kisasa pamoja na uzinduzi wa Kliniki ya meno katika hospitali hiyo sambamba na kuendelea na ujenzi wa jengo la mama na watoto. Jitihada hizi ni kufikia azma ya Serikali ya kuifanya hospitali ya Kivunge kufikia hadhi ya Mkoa. Michoro ya nyumba za madaktari katika hospitali ya Abdullah Mzee Mkoani Pemba imekamilika na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China itasaidia gharama za ujenzi huo. Upembuzi yakinifu kwa ajili ya Ujenzi wa hospitali ya rufaa Binguni umekamilika na matengenezo ya jengo la Taasisi ya Utafiti wa Afya yamefanyika na linatumika. Halikadhalika, michoro ya majengo ya Idara tano ya hospitali hiyo kwa awamu ya kwanza imekamilika na Mshauri elekezi amepatikana.

35. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha michezo, ujenzi wa kiwanja cha michezo cha Mao Tse Tung umekamilika na kimeanza kutumika na ujenzi wa viwanja vitano (5) vya michezo vya Wilaya umeendelea. Ujenzi wa viwanja vya Kishindeni kilichopo Micheweni na Kangani kilichopo Mkoani unaendelea katika hatua za mwisho za kuweka lami. Kiwanja cha Mkoa wa

Mjini Magharibi kimepatikana katika eneo la Kama na kiwanja cha Mkoa wa Kaskazini Unguja kimepatikana katika eneo la Mkokotoni ambapo kazi inayoendelea ni kutayarisha michoro ya viwanja hivyo.

36. **Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya ujenzi wa miji ya kisasa katika maeneo ya Chumbuni na Kwahani yameanza. Kwa upande wa Chumbuni, michoro ya mji pamoja na michoro ya nyumba imekamilika na imewasilishwa Serikalini kwa hatua na maamuzi. Ujenzi huo ambao utakuwa na majengo *(blocks)* 20 utagharamiwa na Benki kutoka China ikiwa ni mkopo wenye riba kati ya asilimia 4 hadi 5 na utalipwa ndani ya kipindi cha miaka 4 baada ya muda wa miaka miwili ya mradi kukamilika (*grace period).* Kwa upande wa Kwahani, Mkandarasi anaendelea na hatua ya michoro na kutayarisha gharama za ujenzi (*Bill of Quantity- BoQ)*. Jumla ya TZS bilioni 20 zitatumika ikiwa ni mkopo kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya ujenzi wa majengo sita hadi saba yatakayokuwa na nyumba 120. Aidha, kampuni ya Lighang ya China itatoa mkopo wa asilimia 80 na Serikali kutoa asilimia 20 ya gharama za ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa majengo mengine yatakayobakia baada ya kukamilika kwa utayarishaji wa BoQ.

**f. Kukuza uwezo wa watu kwa kusomesha wataalamu zaidi**

37. **Mheshimiwa Spika,** Ili kukuza uwezo wa watu kwa kuongeza wataalamu hasa katika fani zenye upungufu ikiwemo afya, nishati na kilimo, jumla ya wanafunzi 308 wamepatiwa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar na kujiunga na masomo hayo. Katika fani ya afya, jumla ya wanafunzi 209 wamepatiwa mafunzo wakiwemo tisa stashahada ya juu, 187 shahada ya kwanza, 12 shahada ya pili na mmoja shahada ya tatu. Kwa upande wa nishati, jumla ya wanafunzi 16 wamepatiwa mafunzo katika masuala ya mafuta na gesi kati yao, 13 shahada ya kwanza na watatu shahada ya pili. Jumla ya wanafunzi 83 wamepatiwa mafunzo katika fani ya kilimo wakiwemo 80 shahada ya kwanza, mmoja shahada ya pili na wawili shahada ya tatu.

**g. Utawala bora na uimarishaji wa Taasisi**

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha utendaji mzuri wa kazi, Ujenzi wa jengo linalojumuisha Wizara sita zikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto; Wizara ya Katiba na Sheria; Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati katika eneo la Gombani Pemba umekamilika

na tayari jengo limefunguliwa tarehe 02 Mei, 2019 na kuanza kutumika. Ujenzi wa nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar katika eneo la Pagali, Chake Chake Pemba unaendelea na upo katika hatua za mwisho kukamilika.

Kwa upande wa ujenzi wa nyumba na mahanga katika kambi za vikosi vya Idara maalum za SMZ unaendelea kwa vikosi vyote vya KMKM, Chuo cha Mafunzo, Kikosi cha Zimamoto, Jeshi la Kujenga Uchumi na Kikosi cha Valantia. Mradi wa Mji Salama umekamilisha uwekaji wa kamera katika Mkoa wa Mjini Magharibi na maeneo muhimu ya Bandari ya Malindi, barabara mbali mbali za mjini na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na kamera hizo zimeanza kufanya kazi. Aidha, ujenzi wa vituo vya uokozi baharini kwa maeneo ya Kibweni (Kituo Kikuu), Nungwi na Mkoani umekamilika na kufungwa vifaa vyote muhimu na kuanza kufanya kazi.

### h. Kuongeza ajira kwa Vijana

39. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya vikundi 40 vinatarajiwa kupatiwa utaalamu na mitaji kwa njia ya mkopo ikiwemo vifaa katika maeneo mbalimbali. Maeneo hayo ni ushonaji, useremala, utengenezaji wa vifaa vya chuma na plastiki, uvuvi, kilimo, ufugaji na ujasiriamali wa kutengeneza sabuni, pilipili hoho na kadhalika. Serikali

inapanga kutumia mifuko ya ajira kwa vijana, mfuko wa SMZ wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na msaada wa Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Falme za Kiarabu kupitia program maalum iliyoanzishwa na Serikali kwa lengo la kupunguza tatizo la mitaji na kuongeza ajira kwa vijana.

40. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia Programu ya Ajira kwa Vijana, shughuli mbali mbali zimefanyika ikiwemo ziara ya kuvitembelea vikundi 128 vya vijana vinavyojishughulisha na shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi, ushoni, ujasiriamali na uchongaji kwa wilaya zote za Unguja na Pemba. Aidha, Tathmini imefanyika kwa vikundi 51 vya kilimo vyenye jumla ya vijana 1,185 na vikundi 26 vya ushonaji vyenye jumla ya vijana 874 wanatarajiwa kunufaika na program hiyo ambapo kwa sasa hatua za manunuzi kwa ajili ya kusaidia mahitaji ya vikundi hivyo zinaendelea.

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ulitowa mikopo 456 yenye thamani ya TZS 677.5 milioni kwa wananchi 2,023; wanufaika wakubwa wakiwa ni vijana. Aidha, jumla ya Dola za Kimarekani milioni 10 zimetengwa kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kwa miaka mitano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa kiwango kama hicho cha Dola za Kimarekani milioni 10 kwa ajili ya kusaidia kupunguza makali kwa wajasiriamali. Makubaliano

kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na UAE yatawekwa saini hivi karibuni.

i. **Kuendeleza tafiti**

41. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kuelewa umuhimu wa tafiti katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii na hatimae kuinua hali za wananchi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejidhatiti katika kutumia utafiti kwa maendeleo kwa kuandaa mazingira mazuri na kubuni tafiti mbali mbali ambazo zitajibu changamoto zinazolikabili Taifa ili kuharakisha kufikia malengo ya Dira ya 2020. Matumizi ya matokeo ya utafiti hupelekea ubunifu ambao hutumika kama kichocheo cha maendeleo na kuinua vipato vya wananchi.

Tume ya Mipango ya Zanzibar inaratibu utekelezaji wa tafiti zifuatazo ambazo ziko katika hatua mbali mbali:- Utafiti juu ya Maradhi yasiyoambukiza (NCD's) kwa watoto; Utafiti wa kuweza kuongeza thamani zao la mwani; Utafiti juu ya Faida/hasara za ongezeko la Idadi ya Watu na Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar; na Utafiti wa uchambuzi wa mahitaji ya wataalamu katika Sekta ya Umma ya Zanzibar. Wizara na Taasisi za Serikali zinafanya tafiti mbali mbali kama zilivyoainishwa katika kitabu cha Agenda za Utafiti Kitaifa cha mwaka 2015-2020. Aidha, watafiti na wataalamu wengine wamekuwa wakiendelea kufanya tafiti kwa mujibu wa miongozo ya Serikali.

**Masuala mtambuka**

**Upelekaji wa Madaraka kwa Wananchi Kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa (Ugatuzi)**

42. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza upelekaji wa madaraka kwa wananchi, Serikali imefanya mapitio ya Sheria saba za sekta zilizogatuliwa ili ziendane na dhana ya ugatuzi. Sheria hizo ni Sheria ya Uvuvi namba 8 ya mwaka 1998, Sheria ya Misitu namba 10 ya mwaka 1996, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 1 ya mwaka 2016, Sheria ya Mifugo namba 11 ya mwaka 1999, Sheria ya Elimu namba. 6 ya mwaka 1982, Sheria ya Afya namba 11 ya mwaka 2012 na Sheria ya Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 2014. Rasimu za mapendekezo ya sheria hizo zimeshatayarishwa na zinaendelea kupata maoni ya wahusika wa sheria hizo. Kukamilika kwa sheria hizo kutasaidia kurahisisha uratibu wa karibu wa masuala ya elimu, afya na kilimo kwa ngazi za Halmashauri, Manispaa, Mabaraza na miji. Ni jukumu la wananchi kufuatilia na kufahamu mabadiliko yaliyomo katika sheria hizo ili kutambua huduma zinazopatikana katika maeneo yao na kuongeza ufanisi wa utendaji wa Serikali za Mitaa.

43. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika mipango yao ya maendeleo, Muongozo wa Uandaaji wa Mpango Shirikishi Jamii kwa kutumia mbinu

ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (Opportunities & Obstacles for Development – O & OD) umeandaliwa. Muongozo huo utakuwa ni nyenzo itakayotumika kuandaa Mipango ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sambamba na hilo, zoezi la kuibua vipaumbele na kuandaa mipango katika Shehia zote 388 za Unguja na Pemba limefanyika pamoja na kuandaa majukumu ya Wasaidizi Makatibu Tawala wa Mikoa na Wasaidizi Wakurugenzi wa Serikali za Mitaa. Serikali inadhamiria kukamilisha kwa haraka mapitio ya sheria zilizofanyiwa kazi na itaendelea kuandaa miongozo mbalimbali inayolenga kuimarisha majukumu ya msingi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**Uzalishaji umeme mbadala**

44. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na jitihada mbali mbali za kuhakikisha kuwa nishati ya umeme inakuwa ya uhakika, nafuu na imara sambamba na kupunguza utegemezi wa nishati ya umeme kutoka Tanzania Bara. Jitihada hizi zinaungwa mkono na Washirika mbali mbali wa Maendeleo ikiwemo Umoja wa Ulaya ambao wamesaidia kufanya utafiti wa nishati ya jua na upepo itakayoiwezesha Zanzibar kutumia umeme mbadala. Baada ya utafiti huo, Serikali imeamua kutilia mkazo umeme wa jua kwa vile matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa ni mazuri. Kufuatilia hali hiyo, Umoja wa Ulaya na Benki ya Dunia wamekubali kuisaidia Zanzibar kuimarisha umeme mbadala katika

maeneo matatu ambayo ni:-

i. Uzalishaji wa umeme wa jua kwa mfumo wa mashirikiano ya sekta ya umma na binafsi: Umeme huo utazalishwa na muwekezaji binafsi wenye Megawati 30 na kuingizwa katika gridi ya Taifa;
ii. Ujenzi wa mtambo wa umeme: Ujenzi wa mtambo wa umeme wenye Megawati 8 hadi 10 unatarajiwa kujengwa kisiwani Pemba;
iii. Kuimarisha mifumo ya nyaya za umeme: Kazi hii itajumuisha ujenzi wa laini za kati na ndogo za umeme pamoja na uwekaji wa transfoma; ununuzi wa betri za kuhifadhia umeme wa jua zenye uwezo wa Megawati 30 na msaada wa kiufundi na kujenga uwezo wa watendaji.

45. **Mheshimiwa Spika,** Benki ya Dunia imeahidi kutoa mshauri elekezi wa umeme ambaye atasaidia maandalizi ya mradi huo hadi hatua ya kupatikana kwa wazabuni. Kukamilika kwa mradi huo, kutasaidia kupunguza tatizo la kukatika kwa umeme iwapo kiwango cha uwezo wa mkonga cha MegaWati 100 kitazidiwa na mahitaji ya umeme yatakayotokana na ukuaji wa Pato la Taifa unaochochewa na shughuli za kiuchumi na kijamii.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2019

### Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

46. **Mheshimiwa Spika,** Kama nilivyotangulia kusema mwelekeo wa ukuaji wa uchumi wa dunia una athari kubwa kwa uchumi wa Zanzibar. Kwa mwaka 2019 matarajio ya kasi ya ukuaji wa uchumi duniani ni wastani wa asilimia 3.5. Kasi ya ukuaji wa Uchumi kwa nchi Zilizoendelea unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 2.0 mwaka 2019, Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 4.5 na nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 3.5.

### Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar 2019

47. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina azma ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wake na kuimarisha ustawi wa maisha ya kila Mzanzibari. Kwa mwaka 2019, Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.8 ambapo mkazo utawekwa katika maeneo sita kama ifuatavyo:

   1. **Kutumia fursa za Uchumi wa Buluu**

48. **Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Buluu unajumuisha shughuli zote zinazoambatana na maeneo ya bahari kama vile uvuvi, utalii, usafiri wa bahari, mafuta na gesi, ufugaji wa mazao ya bahari pamoja na shughuli za kijamii za baharini. Serikali ina azma ya kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kuwekeza zaidi katika rasilimali watu ili tuwe na wataalamu wa kutosha katika eneo hili;
ii. Kuweza kufanya Tathmini ya kuzitambua rasilimali zetu za bahari;
iii. Kuhakikisha kuwa shughuli za baharini zinajumuishwa katika Sera na Sheria pamoja na miongozo katika kupunguza umasikini;
iv. Kuanzisha Idara maalum ili kuratibu vyema masuala yanayohusu uchumi wa buluu. Idara hiyo itafanya kazi kwa karibu sana na sekta zinazohusika moja kwa moja na masuala ya bahari na utajiri mkubwa uliyomo katika maeneo yetu. Idara hiyo pia itasimamia matumizi mazuri ya visiwa vidogo vidogo vilivyozunguka Unguja na Pemba.

## 2. Kutekeleza Sera ya Viwanda ya Zanzibar

49. **Mheshimiwa Spika**, Sera ya Viwanda ya Zanzibar inatoa muongozo katika kuwezesha wajasiriamali

katika kujiongezea vipato vyao kupitia wawekezaji wa nje, ndani na msaada kutoka Serikalini na Washirika wa Maendeleo. Malengo ya Serikali ya kusaidia Maendeleo ya viwanda vya Zanzibar ni pamoja na: -

i. Kutenga ardhi na kuendeleza miundombinu ya shughuli za viwanda katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar katika kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje;
ii. Kuongeza mashirikiano baina ya Vyuo vya Ufundi vya Serikali na wadau wote katika shughuli za uzalishaji viwandani. Kwa mfano kutekeleza programu jumuishi kwa kuongeza uwezo wa washoni wa nguo;
iii. Kuongeza usimamizi wa vyuo kwa ajili ya kutoa taaluma kwa wawekezaji wadogo wadogo na wa kati ili kuongeza vipato vya wajasiriamali hao nchini;
iv. Kuongeza mashirikiano baina ya taasisi na idara zinazoshughulika na masuala ya biashara;
v. Kusimamia fedha za msaada wa Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Falme za Kiarabu na fedha nyengine ambazo zitatolewa kwa wajasiriamali ili kuendeleza miradi yao.

### 3. Kuunganisha Sekta ya Utalii na sekta nyengine za uzalishaji

50. **Mheshimiwa Spika** Sekta ya utalii inatoa mchango mkubwa katika ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar. Sera za Serikali zimelenga katika kuunganisha sekta ya utalii na sekta nyengine za uzalishaji ili utalii uweze kuwa na manufaa zaidi. Hii ni pamoja na kuunganisha sekta ya kilimo na Utalii Kwa Wote kwa kuanzisha utalii wa kilimo 'agri-tourism' na mambo yafuatayo yataendelea kufanyiwa kazi: -

**a. Ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya programu ya mahoteli inakusudia**

i. Kuwawezesha wanavijiji wanaoizunguka hoteli kuuza bidhaa za chakula na kazi za mkono kwa wageni;

ii. Kuendelea kutolewa taaluma na mbegu bora kwa bidhaa zinazohitajika katika mahoteli;

iii. Kuendelea kutolewa mafunzo zaidi kwa Wazanzibari ili waweze kuajirika katika sekta ya utalii;

iv. Kuwawezesha wajasiriamali kuzalisha bidhaa ambazo zinahitajika katika soko la utalii zikiwemo: maziwa na mtindi.

b. **Programu mjumuisho ya maendeleo ya sekta ya utalii inakusudia**

i. Kuitangaza zaidi Zanzibar kwa kutumia mifumo ya kidigitali kama “google” kwa madhumuni ya kuiweka nchi yetu kwenye ramani ya dunia;

ii. Kuimarisha maeneo ya vivutio vya utalii vilivyopo kama vile shamba na viungo, urithi wa utamaduni, na biashara;

iii. Kukiwezesha chuo kikuu cha Taifa (SUZA) kutoa wataalamu katika fani ya utalii;

iv. Kuongeza uhusiano baina ya utalii na kilimo ikiwemo kupata bidhaa za chakula kutoka kwa mkulima mzawa;

c. **Wazawa kuunganishwa na sekta ya utalii**

i. Kuongeza usarifu wa bidhaa za chakula na kushajihisha viwanda vya usambazaji wa vyakula kwa mahoteli na ndege za kimataifa;

ii. Kuitangaza Zanzibar kama ni sehemu ya kutembelea kwa kutoa punguzo kwa mashirika ya ndege ili kuongeza uhusiano na kuongeza idadi ya watalii nchini;

iii. Kuitumia Miongozo ya Tafsiri ya Biashara ya mwaka 2016 (Trade transaction Regulations

of 2016) ambayo inawataka wauzaji wa bidhaa na huduma kwa mkopo kuingia katika makubaliano baina ya pande mbili;

iv. Mnunuaji wa bidhaa zilizozalishwa ndani apatiwe unafuu wa kodi kutoka katika bidhaa hiyo.

### 4. Kuanzisha Viwanda vidogo vidogo

51. **Mheshimiwa Spika,** Viwanda vidogo vidogo vinajumuisha takribani viwanda vya usarifu na uhifadhi wa bidhaa ya chakula na zisizo za chakula. Zanzibar inayo nafasi kubwa kuongeza uzalishaji ambayo italeta mafanikio makubwa katika kukuza uchumi wake na mambo yafuatayo yatapewa mazingatio: -

i. Kuvutia uwekezaji binafsi katika uvuvi wa bahari kuu, ufugaji wa samaki, kuongeza thamani zao la mwani na ushajihishaji wa kilimo cha asili;

ii. Kuendelezwa kwa vituo vya utafiti wa Afya, Kilimo, Mifugo pamoja na tafiti za vyakula na vinywaji na kufanyiwa kazi mapendekezo yatokanayo na tafiti hizo kwa jamii;

iii. Kuitangaza Zanzibar kwa kutengeneza tovuti, alama ya ubora wa bidhaa za Zanzibar na kushirikisha vyombo vya kijamii katika kuitangaza Zanzibar;

5. **Kutafuta fursa zinazopatikana katika visiwa vidogo vidogo vilivyopo Zanzibar**

52. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa hali ya kijiografia Zanzibar imezungukwa na visiwa vidogo vidogo vilivyo na sifa za kipekee. Visiwa hivyo vidogo vidogo vinatumika kwa shughuli mbali mbali zikiwemo makaazi, kambi za wavuvi (dago), maeneo ya kilimo na shughuli za utalii wa kwenda na kurudi au hoteli za kulaza wageni. Visiwa vidogo vidogo 57 bado havijatumika ipasavyo katika kukuza uchumi wa nchi ikiwemo kuvutia watalii wa daraja la juu. Visiwa hivyo vina rasilimali tafauti za kimaumbile ikiwemo wingi wa rutuba kwa uzalishaji wa mazao, viumbe hai, fukwe, misitu ya asili na ni kivutio kikubwa cha utalii. Kati ya visiwa hivyo visiwa 9 tu ndio vina uwekezaji kwa mujibu wa mikataba navyo ni:

i. The Achers Zanzibar Limited - Kisiwa cha Mnemba;
ii. Chumbe Island Coral Park - Kisiwa cha Chumbe;
iii. Leisure Hotel Changuu Island Zanzibar - Kisiwa cha Changuu;
iv. Leisure Hotel Bawe Island Zanzibar - Kisiwa cha Bawe;
v. Dodia Diving Center Company Limited Zanzibar - Kisiwa cha Uzi;

vi. Rihla Company Limited Zanzibar - Kisiwa cha Kwale;
vii. Rihla Company Limited Zanzibar -Kisiwa cha Niamembe;
viii. Fundo Lodge Limited Zanzibar - Kisiwa cha Fundo;
ix. Oxygen Holding Company Limited Zanzibar -Kisiwa cha Uvinje.

Mikataba yote hiyo ya uwekezaji katika visiwa hivyo itapitiwa na kurekebishwa pale panapoonekana ipo haja.

**53. Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa mwaka 2019/20 imekusudia kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kuzipitia upya kodi za ardhi za visiwa ili zisaidie ustawi wa wananchi walio karibu na maeneo ya mradi. Mapitio hayo yatazingatia rasilimali ya ardhi, eneo na tija inayopatikana;
ii. Kuwahamasisha wawekezaji wa nje na wa ndani ili kutumia fursa ya visiwa kama ni maeneo ya uwekezaji;
iii. Kufanya tafiti za kina kwa kuanzia visiwa vya Misali, Fungu Mbaraka, Hamisi, Usubi na Pungume ambavyo vina rasilimali nyingi zaidi na visiwa vyengine kadiri hali itakavyoruhusu kwa kuangalia fursa zinazopatikana katika visiwa hivyo;

iv. Kufanya mapitio ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya vivutio na michezo ya watalii pamoja na kuwatambua wanaolipa tozo ya michezo hiyo.

**Shabaha na Malengo ya Uchumi Kwa mwaka 2019-2021.**

**54. Mheshimiwa Spika,** Shabaha na malengo ya uchumi kwa kipindi cha miaka mitatu ni kama ifuatavyo:-

i. Kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kwa miaka mitatu inategemewa kuwa baina ya asilimia 8 mpaka 10;
ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kuwa wastani wa chini ya asilimia 5 kwa kipindi cha miaka mitatu;
iii. Mapato ya ndani kwa kipindi cha miaka mitatu inakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 26.4 ya Pato la Taifa mwaka 2019/21 kutoka asilimia 24.2 kwa mwaka 2018/19;
iv. Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu yanakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 39.4 ya Pato la Taifa mwaka 2019/21 kutoka wastani wa asilimia 38 mwaka 2018/19;
v. Kwa kipindi cha miaka mitatu inakadiriwa kupunguza nakisi ya bajeti kufikia wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2019/21 kutoka wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2018/19 na;

vi. Kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu;

vii. Kujitegemea zaidi wenyewe na kupunguza utegemezi kutoka nje.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2019/20

**55. Mheshimiwa Spika,** wakati Serikali ikiendelea kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, hivi sasa imeanza kufanya tathmini ya utekelezaji kwa kipindi kilichopita na kuandaa Dira mpya kwa kipindi kijacho. Kama tujuavyo, Dira ya Maendeleo iliyozinduliwa mwaka 2020 inakaribia kumalizika muda wake, hivyo kuna haja ya kufanya tathmini na kuandaa dira nyengine itakayotoa mwelekeo kwa kipindi kirefu kijacho kuanzia mwaka 2021 hadi 2050. Mabadiliko ya kidunia, kikanda na kitaifa yaliyotokea kwa muda wa miaka 20 iliyopita yanahitajika kufanyiwa tathmini ili kujua athari yake na namna ya kuzingatia katika Dira mpya. Aidha, mwelekeo mpya na vipaumbele vya uchumi wa Zanzibar wa uwezekano wa kuwepo mafuta na gesi, mabadiliko ya sera na mipango ya kimataifa, mageuzi ya sayansi na teknolojia na mabadiliko ya tabianchi yanahitaji sera na mikakati mipya ya kutekeleza. Mahitaji hayo ya kitaifa na masuala ya kimataifa yamechangia haja ya kufanyika tathmini na kuandaliwa upya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar.

56. **Mheshimiwa Spika,** Serikali tayari imeanza matayarisho ambapo Kamati ya Tathmini na Kamati ya Dira zimeshaundwa zitakazosaidiwa na Kamati za Ufundi. Mafanikio na changamoto za utekelezaji wa Dira zitaainishwa ili kurahisisha uandaaji wa dira mpya. Nina matumaini ya kuwa wataalamu wa fani mbali mbali, wadau wa maendeleo na jamii kwa ujumla watashiriki kikamilifu na kutoa maoni yao ili Zanzibar iwe na maendeleo endelevu kwa watu wote. Ni jukumu la kila mmoja wetu kwa njia tafauti na kwa nia ya kushiriki kikamilifu katika kuandaa, kubuni na kutekeleza maeneo yenye tija kwa kipindi kilichobaki cha Dira; ili nchi yetu ifikie uchumi wa kipato cha kati katika mwaka 2020 ikiwa ni dhamira kuu ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020 na Mikakati ya Kitaifa ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar.

## Vipaumbele vya Kitaifa kwa mwaka 2019/20

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka 2019/20 vipaumbele vya kitaifa vimejikita katika kutekeleza MKUZA III na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 kwa lengo la kufikia azma ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020. Sekta kuu za kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi zikiwemo Kilimo, Utalii, Miundombinu, Elimu na Afya zitaendelea kupewa msukumo unaostahiki kupitia utekelezaji

wa programu na miradi mbali mbali ya maendeleo. Kwa kuzingatia umuhimu na faida zitakazopatikana, vipaumbele vya mwaka 2019/20 vimepangwa katika makundi mawili kama ifuatavyo:

## I. Vipaumbele vya Juu

58. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kutekeleza vipaumbele vya mwanzo ambapo mkazo mkubwa utawekwa katika kutekeleza miradi ifuatayo:

a) Ukamilishaji wa jengo la abiria la uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzibar (Terminal III);

59. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa jengo la abiria la uwanja wa ndege katika kukuza uchumi, Serikali imedhamiria kukamilisha jengo hilo kwa kutumia fedha zake wenyewe kufuatia kutokamilika kwa makubaliano ya upatikanaji wa mkopo kutoka Benki ya Exim ya China.

b) Kuanza ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri;

60. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inakusudia kukamilisha upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi ili kuimarisha mapato na kupunguza msongamano wa meli, abiria na mizigo katika bandari ya Malindi.

c) Kuanza ujenzi wa Hospitali Mpya ya rufaa ya Binguni;

61. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kupeleka huduma nyengine za rufaa katika Hospitali ya Binguni ambayo itakuwa na huduma za hospitali pamoja na kufundishia madaktari na wataalamu mbali mbali wa afya. Kwa mwaka 2019/20, Serikali imepanga kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa hospitali hiyo itakayohusisha majengo ya Idara tano.

d) Kuanza ujenzi wa Mahakama Kuu huko Tunguu;

62. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuimarisha utawala bora kupitia upatikanaji wa haki za raia, Serikali imekusudia kuanza ujenzi wa Mahakama Kuu ya kisasa katika eneo la Tunguu Unguja. Hali hii inafuata baada ya kupatikana mkandarasi wa ujenzi kupitia hatua za manunuzi ambazo hivi sasa ziko katika hatua za mwisho.

e) Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja;

63. **Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa barabara ya Ole Kengeja umeendelea kwa takriban miaka saba hadi sasa. Barabara hii yenye urefu wa kilomita 35 inayounganisha wananchi wa Wilaya za Chake Chake na Mkoani kwa upande wa

Mashariki ni muhimu katika kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo. Serikali imekusudia kukamilisha ujenzi huo unaoendelea katika hatua mbali mbali.

f) Kuimarisha ulinzi na usalama nchini.

64. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya kiuchumi na kijamii yanaweza kufikiwa pale penye amani na usalama wa kutosha. Bila ya amani hakuna maendeleo. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha amani katika maeneo yote ya Unguja na Pemba; ili kuleta ustawi wa wananchi wake. Hatua mbali mbali zitachukuliwa ikiwemo uwekaji wa kamera za ulinzi katika maeneo ya miji na kusimamia kwa nguvu zake zote ili amani na usalama uweze kushamiri katika visiwa vyetu. Aidha, usalama utaimarishwa kwa utekelezaji wa shughuli mbali mbali zikiwemo ununuzi wa boti za uokozi na chumba cha huduma za uzamiaji (decompression chamber).

## II. Vipaumbele vyengine

65. **Mheshimiwa Spika,** vipaumbele vyengine vya Serikali kwa mwaka 2019/20 ni kama vifuatavyo:

a) Kuimarisha ajira kwa vijana kupitia utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana, Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Falme za Kiarabu na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi;

b) Kuimarisha hospitali za Kivunge na Wete kuwa katika hadhi ya mkoa.

c) Kuliimarisha eneo la Bandari ya Mangapwani kwa ukamilishaji wa upembuzi yakinifu wa bandari ya mafuta na gesi; ujenzi na uwekaji wa miundombinu ya msingi ikiwemo barabara, maji na umeme; na ujenzi wa matangi ya kuhifadhia mafuta;

d) Kukuza taaluma katika sekta ya mafuta na gesi;

e) Kuendelea na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi;

f) Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Bububu – Mahonda – Mkokotoni;

g) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi na makambi ya vikosi vya Idara maalum za SMZ;

h) Utekelezaji wa mpango wa ugatuzi nchini;

i) Utekelezaji wa ujenzi wa majengo ya Ofisi za Serikali.

## RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2019/20

66. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20, Mpango wa Maendeleo unalenga kutekeleza jumla ya programu 27 na miradi 48 ya maendeleo. Jumla ya TZS 577.02 bilioni zitatumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ikiwa ni upungufu wa TZS 35.93 bilioni sawa na asilimia 5.86 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2018/19 ya TZS 612.95 bilioni.

Serikali imepanga kutumia fedha zake TZS 182.40 bilioni sawa na asilimia 31.61 ya Bajeti ya Maendeleo ikiwa ni ongezeko la TZS 33.65 bilioni sawa na asilimia 22.6 ya Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2018/19 ya TZS 148.75 bilioni. Kati ya fedha za Serikali (TZS 182.40 bilioni), TZS 116.44 bilioni ni kwa programu na miradi ya kimkakati, yenye mikataba au dhima 'Commitment' na TZS 65.96 bilioni kwa miradi mengine. Aidha, jumla ya TZS 394.62 bilioni sawa na asilimia 68.39 ya bajeti ya Maendeleo zimepangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 95.52 bilioni ni ruzuku na TZS 299.10 bilioni ni mikopo. Fedha hizo ni upungufu wa TZS 69.58 bilioni sawa na asilimia 14.99 ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwa mwaka 2018/19 zenye jumla ya TZS 464.2 bilioni.

## HITIMISHO

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Hotuba yangu hii kwa mara nyengine napenda niishukuru Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi iliyo chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed (Dimwa), Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae na Mheshimiwa Bahati Khamis Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati. Aidha, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo chini ya uwenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Hamida Abdalla Issa na Waheshimiwa wajumbe wote kwa maoni na ushauri waliotupatia kupitia Kamati hizi mbili yamesaidia kuimarisha Mpango wetu wa Maendeleo ili kuwa na tija kwa wananchi wote.

68. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, naomba kutoa shukurani za dhati kwa watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na aliyekuwa Katibu Mtendaji Ndugu Juma Hassan Reli na Katibu Mtendaji wa sasa Ndugu Mwita Mgeni Mwita kwa umakini wao katika hatua zote hadi kupatikana kwa Hotuba hii.

69. **Mheshimiwa Spika,** shukurani za kipekee zimwendee Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mussa Omar na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Aidha, natoa shukurani

za dhati kwa Makatibu Wakuu wa Wizara za SMZ na Watendaji wao kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika matayarisho ya Hotuba hii. Ni matumaini yangu kwamba tutaendelea kushirikiana katika kutekeleza mipango yetu na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa kazi za kila siku.

70. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nisisitize suala zima la Uzalendo. Hii ni muhimu kwa wananchi kuwa nao na kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni na kutekeleza miradi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu sambamba na uwajibikaji ndani ya utumishi wa umma. Mfumo wa ufuatiliaji kwa kupima matokeo (*balanced scorecard*) ulioanzishwa unatoa ushindani wa Taasisi za Umma kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kupelekea wadau kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Nitoe wito kwa wananchi kufanya juhudi ya kutekeleza kwa vitendo malengo ya Dira na kuhakikisha yanafikiwa katika kiwango cha kuridhisha ifikapo mwaka 2020.

71. **Mheshimiwa Spika**, Washirika wetu wa Maendeleo waliotusaidia kufanikisha Mpango wetu wa Maendeleo wanahusisha Mashirika ya Kitaifa, Kimataifa na Nchi Wahisani na kwa aina ya kipekee naomba kuwashukuru kwa misaada ya kifedha na kiutaalamu wanaoendelea kutupatia wakiwemo ACRA, AGRA, AFYA BORA,

AfDB, HOPELAND UNIVERSITY, BADEA, CARE AUSTRIA, CHINA, CANADA, CIDA, COSTECH, DFID, EAC, EGH, EGYPT, EU, EXIM BANK CHINA, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, GPE, INDIA, ICAP, IFAD, ILO, IMF, JAPAN, JICA, MFUKO WA MAENDELEO WA UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE), KOREA, KUWAIT, MILELE FOUNDATION, NMB, NORWAY, OFID, ORIO - NETHERLAND, OMAN, OPEC, PMI, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, SWEDEN, THPS, UK, UNDP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, URT, USAID, UN WOMEN, WORLD BANK na WHO.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa Baraza lako tukufu lipokee na lijadili Mwelekeo wa Uchumi 2019 na kuidhinisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/20.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.

**BALOZI MOHAMED RAMIA ABDIWAWA (MBM)**
**Waziri,**
**Wizara ya Fedha na Mipango**
**Zanzibar**